**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

---

Ofisi ya Bunge,
Idara ya Kamati za Bunge,
S.L.P. 941,
**DODOMA**

*10 MEI, 2017*

# YALIYOMO

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1

1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA ........ 1

1.1 MAJUKUMU YA KAMATI ........ 1

1.2 MUUNDO WA TAARIFA ........ 1

**SEHEMU YA PILI** ........ 3

2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI ........ 3

2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI ........ 3

3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 ........ 5

4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 ...... 8

4.1 MRADI WA MAJI KUTOKA ZIWA VIKTORIA HADI SHINYANGA ........ 8

4.2 UJENZI WA TANKI LA MAJI KATIKA MJI WA KLISHAPU ........ 8

4.3 MRADI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA WA ZIWA VIKTORIA AWAMU YA PILI (LV WATSAN II) 9

4.4 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ........ 10

4.4.1 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI FUNGU 05 ........ 10

4.4.2 WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI FUNGU 49 ........ 14

4.4.3 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 ........ 18

**SEHEMU YA TATU** ........ 20

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ........ 20

6.0 HITIMISHO ........ 27

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

### 1.1 MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Maji ina mafungu mawili ambayo ni:-

- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 - na
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji - Fungu 49.

### 1.2 MUUNDO WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

(e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

## 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Toleo la 2005 imeipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani saba (7) ya kipaumbele. Maeneo hayo yalijumuisha ushauri kuhusu:-

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati;

(b) Mapendekezo ya kuongeza tozo ya shilingi hamsini kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli ili kutunisha mfuko wa maji;

(c) Hujuma dhidi ya miundombinu ya maji;

(d) Umuhimu wa Serikali na Taasisi zake kulipa Ankara za maji kwa wakati ;

(e) Upungufu wa wataalamu katika sekta ya maji;

(f) Umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua na;

(g) Umuhimu wa matumizi ya rasilimali maji katika kuongeza tija na uboreshaji wa Sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na kufanyiwa kazi isipokuwa ushauri kuhusu:-

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; kwani hadi kufikia mwezi Machi 2017 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 19.8** tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Hali iliyopelekea Wizara kushindwa kutekelezwa kwa miradi mingi ya maendeleo.

(b) Kutoongezwa kwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya dizeli na petroli kutoka shilingi 50 ya sasa hadi kufikia shilingi 100, ushauri ambao ulipokelewa na Serikali lakini haujatekelezwa kwa maelezo kwamba ushauri huu unaendelea kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ushauri huo kutotekelezwa, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa mwenendo huu wa kutotoa fedha zote za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri kwa kiasi kikubwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara. Vilevile kutoongezwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya petrol na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100) kunaathiri ufanisi wa Mfuko wa Maji.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Machi, 2017 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi tarehe 31 Machi, 2017.

**3.1** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Maji na Umwagiliaji- Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **939,631,302,771**. Kati ya fedha hizo shilingi **7,075,948,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **17,361,417,000** ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi **915,193,937,771** zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

**3.2** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji **-** Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **39,876,143,028** kati ya fedha hizo shilingi **4,506,613,600** ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi **4,206,825,600** ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi **299,788,000** ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikuwa shilingi **35,369,529,428** kati ya hizo shilingi ni **6,000,000,000** ni fedha za ndani na shilingi **29,369,529,428** ni fedha za nje.

**3.3** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2017 Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za matumizi mengineyo shilingi **3,424,260,246.43** sawa na **asilimia 48**, na mishahara shilingi **10,862,692,720** sawa na **asilimia 62** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi 2017 zilikuwa shilingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** ya fedha zote za bajeti ya maendeleo.

**3.4** **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 hadi kufikia Machi, 2017 fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi **122,394,224** ambayo ni sawa na **asilimia 40.8**. **na shilingi 2, 409, 935, 000** zilitolewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **2,986,101,292** zilitolewa ambazo ni sawa na **asilimia 8.4** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi **2,339,980,000** sawa

na **asilimia 39** ya fedha za ndani na shilingi **646,121,292** sawa na **asilimia 2.2** ya fedha za nje.

3.5 **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika (2016/2017) jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa ni shillingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** mwenendo huu ni wa kusikitisha na hasa ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa. Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge sababu za kutopeleka fedha kadri zilivyoidhinishwa na Bunge.

3.6 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi **550,005,000** Hadi kufikia Machi 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **467,633,790** ambayo ni sawa na **asilimia 85** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo lakini inahimiza kuongeza juhudi za ukusanyaji ili kufikia malengo iliyojiwekea.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2016/2017). Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

## 4.1 MRADI WA MAJI KUTOKA ZIWA VIKTORIA HADI SHINYANGA

**Mheshimiwa Spika,** katika mkoa wa Shinyanga Kamati ilikagua mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Shinyanga, Mwadui, Kishapu na Maganzo, uliotengewa shilingi **1,000,000,000** na fedha zote kutolewa kwa wakati. Katika ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa, mradi huu umetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na thamani ya fedha imetumika ipasavyo.

## 4.2 UJENZI WA TANKI LA MAJI KATIKA MJI WA KLISHAPU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua ujenzi wa tanki kubwa la maji katika mji wa Kishapu ilibaini kwamba hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa tanki hilo ni ya kuridhisha. Aidha, kutokana na mji wa Kishapu kutokuwa na miundombimu ya usambazaji maji, Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti itakayowezesha Halmashauri kujenga kwa wakati miundombinu itakayokidhi kusambaza maji hayo pindi mradi huu utakapokamilika.

## 4.3 MRADI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA WA ZIWA VIKTORIA AWAMU YA PILI (LV WATSAN II)

**Mheshimiwa Spika,** katika mkoa wa Mwanza, Kamati ilikagua mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Ziwa Viktoria Awamu ya Pili (LV WATSAN II) mradi unaotekelezwa katika Wilaya ya Sengerema. Mradi ambao unagharimu dola za kimarekeni **milioni 30.4** na umekuwa ukitekelezwa kwa awamu tangu mwaka 2011 na unategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu, ulitengewa shilingi **1,804,358,000,** hadi kufikia mwezi Machi, 2017, mradi ulikuwa umepokea shilingi **614,966,347** ambazo ni sawa na **asilimia 34** ya fedha iliyotengwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizosalia kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kuwezesha mradi huu kamilika kwa muda uliopangwa ambao ni Desemba 2017**.** Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji kwenye vijiji vilivyolengwa kufikiwa na mradi huu. Lakini pia kubuni na kutekeleza miradi ya aina hiyo katika maeneo mengine ambayo kuna maziwa, mabonde na mito ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kuondokana na uhaba mkubwa wa maji safi na salama ambayo imekuwa ni kero ya muda mrefu.

## 4.4 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 tarehe 30 na 31 Machi , 2017. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi umezingatia Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu II) na Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010 pamoja na Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

### 4.4.1 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI FUNGU 05

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 05 linahusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ambapo pamoja na majukumu mengine Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inajukumu la kuhakikisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inatekelezwa kwa vitendo.

4.4.1.1 **Mheshimiwa Spika,** Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inahimiza umuhimu wa kuendeleza eneo kubwa lililopo nchini linalofaa kwa umwagiliaji

kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kwenye mazao ya chakula, biashara, malisho na kilimo cha majani[1]. Kwa muktadha huu, maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018 na utekelezaji wa bajeti unalenga kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda.

**4.4.1.2** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **24,158,893,232**. Kati ya fedha hizo, shilingi **20,103,412,150** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **4,055,481,082** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, hadi kufikia Juni 2018, Tume ya Taifa inatarajia kukusanya shilingi **15,500,000** kutokana na usajili wa vyama 100 vya umwagiliaji.

[1] Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zinazoombwa zinakusudiwa kutumika kutekeleza pamoja na kazi zingine vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuendeleza ujenzi wa mabwawa ya Dongobeshi (Manyara), Itagata (Manyoni) na kujenga bwawa jipya la Tlawi ( Mbulu);

(b) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa skimu za Igenge (Misungwi), Kirya (Mwanga), Kongogo (Bahi), Endagaw (Hanang), Mbogo na Kigugu (Mvomero);

(c) Kujenga na kukarabati skimu za Segeni (Rufiji), Msolwa Ujama, Njage na Mkula (Kilombero) na Mvumi ( Kilosa); na

(d) Kujenga uwezo wa vyama 442 vya wamwagiliaji na wataalamu kuhusu uendeshaji skimu za umwagiliaji.

**4.4.1.3** **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo fedha nyingi zimekuwa zikitengwa kwenye matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na matumizi ya kawaida, jambo ambalo limekuwa likipongezwa na Kamati, hata hivyo hali ni tofauti wakati wa utekelezaji wa bajeti. Kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2016/2017

kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganisha na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, baadhi ya miradi ya maendeleo haikupata fedha yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yanathibitishwa na jedwali lifuatalo linaloonyesha muhtasari wa Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2016/2017

| **Kifungu** | **Idara/ Kitengo** | **Bajeti iliyoidhinisha 2016/2017** | **Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Machi,2017** | **% ya fedha iliyotolewa** |
|---|---|---|---|---|
| 2002 | Ujenzi na Usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji | 16,562,474,928 | 497,000,000 | **3 %** |
| 2003 | Ufatifi na Uhamasishaji wa Teknolojia za Umwagiliaji | 200,000,000 | 00 | **0 %** |
| 2004 | Huduma za uendeshaji | 845,568,000 | 00 | **0 %** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | na uwezeshaji wa umwagiliaji | | | |

**Chanzo cha taarifa**: Randama ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu - 05 Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, tafsri ya jedwali hili ni kwamba Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kulipa Watumishi wa umma mishahara pasipo kuwawezesha Watumishi kutekeleza majukumu yao kwani kazi nyingi zinazotekelezwa na Tume ya Umwagiliaji ni kazi za vitendo ( *field work)* hivyo kukosekana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kunapelekea mipango iliyopangwa kutotekelezwa.

### 4.4.2 WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI FUNGU 49

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inaeleza kuwa maji ni bidhaa muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Hivyo upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote[2]. Kwa kutambua hilo ndio maana swala la maji limewekewa mkazo katika malengo ya mahususi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu.

[2] Sera ya Maji ya Mwaka 2002

Lengo la sita la maendeleo endelevu linadhamiria kuona kuna upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ifikapo 2030.

**4.4.2.1 Mheshimiwa Spika**, juhudi za upatikanaji wa maji safi na salama zinaweza kuonekana katika kila hatua ya MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania) , Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Tanzania Development Vision 2025*), Matokeo Makubwa sasa (*Big Results Now*) na katika ilani zote za uchaguzi wa vyama vya siasa.

**4.4.2.2 Mheshimiwa Spika,** juhudi zote hizo zinadhihirisha kwamba Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini umethibitika kuwa mgumu hususan maeneo ya vijijini ambapo takwimu zinaonyesha ni **asilimia 46% tu** ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata maji safi na salama na **asilimia 74%** kwa wakazi wa mjini.

**4.4.2.3 Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 inatarajiwa kwenda kutekeleza miradi itakayosaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na

salama ili kuhakikisha kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ni:-

(a) Kuwa na huduma bora ya maji kwa wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;

(b) Huduma bora za maji vijijini kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na

(c) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuvilinda, kuvitunza, kuviendeleza na kutafuta vyanzo vipya vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na vipaumbele hivyo, bajeti hii pia itatekeleza malengo ya muda wa kati kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kwa **asilimia 85** kwa wakazi wa vijijini na **asilimia 95** kwa maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2020;

(ii) Kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta **468,338** za sasa hadi hekta **1,000,000** ifikapo 2021;

(iii) Kuhakikisha rasilimali za maji zinatunzwa, zinasimamiwa, na zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi; na

(iv)Kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza Watumishi wa Sekta ya Maji na Umwagiliaji ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

4.4.2.4 **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 24,457,459,705** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 6,636,518,705** sawa na **asilimia 27** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya kawaida (*Other Charges*) na **shilingi 17,820,941,000** sawa na **asilimia 73** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya Watumishi.

4.4.2.5 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 623,606,748,052.** Kati ya fedha hizo, shilingi **408,617,643,052** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani na shilingi **214,989,105,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje**.** Aidha, fedha zingine za nje shilingi 78,420,000,000 zimetengwa kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI kwa ajili ya miradi ya maji na kampeni za maji na usafi wa mazingira vijijini.

**4.4.2.6** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia fungu 49 imepanga kukusanya shilingi **590,005,000** itakazozipata kutokana na makadirio ya kukusanya maduhuli yatakayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji visima vya maji na tozo mbalimbali zitakazotozwa kwa wateja watakaopata huduma za maabara za ubora wa maji.

**4.4.2.7** **Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeendelea kutenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 49 limetengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi **408,617,643,052** ambayo ni sawa na **asilimia 66** ya fedha zote za maendeleo. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinihwa zinatolewa kwa wakati.

### 4.4.3 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo,

tathimini ya Kamati katika kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umebaini kwamba fedha zinazoombwa hazikidhi mahitaji makubwa ya Maji kama yalivyoelezwa katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Awamu ya I&II) ambayo imebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji, viwanda, usafirishaji na uchukuzi na kupunguza umaskini.

**4.4.3.1** **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kwamba, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo na kushindwa kuzitoa kama zilivyoidhinishwa. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha shilingi **915,193,813,609** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** tu ya fedha zote za bajeti ya maendeelo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

## SEHEMU YA TATU

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwenye maeneo sita (6) yafuatayo:-

### 1) Mtiririko wa Fedha za miradi ya maendeleo usiokuwa na uhakika

**Mheshimiwa Spika,** upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na Serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Maji na Umwagiliaji, Kamati inashauri Serikali kutekeleza adhima ya kuhudumia wananchi kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kadri zilivyoidhinishwa na Bunge.

### 2) Kilimo cha Umwagiliaji na uhusiano wake na uchumi wa viwanda

**Mheshimiwa Spika,** uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi umepelekea maeneo mengi ya nchi kuwa kame, hivyo kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kukidhi mahitaji ya chakula cha kutosheleza nchi, hivyo kilimo cha umwagiliaji kina nafasi kubwa ya

kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kupatikana ziada itakyouzwa nje ya nchi na kuliongezea Taifa fedha za kigeni. Hivyo, Kamati inashauri Serikali:-

(a) Kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iweze kujenga miundombinu ya umwagiliaji itakayowezesha Taifa kuwa na kilimo chenye tija katika maeneo mbalimbali nchini kwa mwaka mzima;

(b) Kuainisha/kutenga kanda maalum za kipaumbele zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

(c) Kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Umwagiliaji. Uhakika wa upatikanaji fedha za Mfuko wa Umwagiliaji utapelekea kutekeleza azma ya Serikali ya kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta **468,338** za sasa hadi kufikia hekta **1,000,000** ifikapo 2021.

**3) Uchimbaji na Ukarabati wa Mabwawa na Visima kwenye maeneo kame nchini**

**Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye

mabwawa na visima vilivyochimbwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwasababu ujenzi wa mabwawa ukikamilika utasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, majumbani, mifugo, viwandani na uzalishaji wa umeme.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa ujenzi wa mabwawa nchini mabwawa ya Lugoda (Ndembera), Farkwa (Dodoma), Mbangala (Songwe) na Dongwe (Kiteto) umekuwa ukisuasua. Aidha, kutokana na mabiliko ya tabianchi visima vingi vya asili na vilivyojengwa na Serikali katika maeneo mbalimbali nchini vimekauka na hakuna hatua za haraka zilizochukuliwa kwa maelezo kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa miradi ya visima na mabwawa kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishangazwa na maelezo haya kwani wapo wawekezaji wenye teknolojia rahisi na ya kisasa na wana fedha za kuwekeza katika sekta ya Maji kwa mikopo nafuu na misaada. Kwa mfano; Kamati ilikutana na kampuni ya ***Investglobal and Associate*** ambao wako tayari kuingia ubia na Serikali katika ujenzi wa miradi ya visima kwa kutoa mkopo wenye masharti

nafuu kwa kipindi cha malipo ya kati ya **miaka 10-20**, mkopo utakaoanza kulipwa kuanzia **miaka 2-3** baada ya mradi kukamilika na **asilimia 35** ya mkopo huo ni msaada. Vilevile kampuni hii itabeba dhamana ya visima hivyo kuendelea kutoa maji kwa kipindi cha miaka kumi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na uhaba wa maji katika maeneo kame nchini ikiwa ni pamoja na kuepukana na changamoto zilizopo za miradi mingi ya visima kutotoa maji na mabwawa kukauka muda mfupi baada ya uchimbaji na hivyo kupoteza fedha za Serikali, Kamati inaishauri Serikali kuondokana na urasimu usiokuwa wa lazima na kutumia fursa za kushirikiana na sekta binafsi (*Private Public Partnership*)kwa kuchukua hatua ili kujiridhisha na masharti ya mikopo, misaada na faida zinazoonyesha kuambatana na wadau wa sekta binafsi waliotayari kushirikiana na Serikali.

**4) Mradi wa kimkakati wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni wazo lililoasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere miaka ya 1980. Bwawa la Kidunda lina umuhimu mkubwa katika uhai wa Mto Ruvu kwani kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa hili kutawezesha mikoa ya Dar es salaam na Pwani kuwa na uhakika wa maji kwa kipindi chote cha

mwaka mzima pamoja na kuzalisha umeme wa **megawati 20** ambao utachochea pamoja na mambo mengine utekelezaji wa adhma ya Tanzania ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** usanifu wa bwawa hili ulianza mwaka 2010 ulikamilika mwaka 2012 ambapo gharama ya ujenzi wa mradi inatarajiwa kuwa **Dola za Marekani milioni 215** sawa na shilingi **bilioni 430**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa bwawa hili hatua mbalimbali za kutafuta vyanzo vya fedha za kutekeleza mradi huo zimekuwa zikichukuliwa, hata hivyo upatikanaji fedha za uhakika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili umekuwa wa kusuasua.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa, tarehe 2 Machi, 2015, Tume ya Mipango iliiandikia barua Wizara ya Fedha na kuishauri Serikali kuwa ujenzi wa bwawa la Kidunda ni moja ya vipaumbele vya Serikali. Aidha, Tume ya Mipango iliishauri Serikali kuendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo ya China ili kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya *Exim* China imeonyesha utayari wa kugharamia mradi huu ambao ujenzi wake utagharimu **Dola za Marekani milioni 215** na benki imetoa tarehe ya mwisho ya kusubiri majibu ya Serikali kuwa 17 Agosti, 2017 endapo muda huu utapita bila majibu ya Serikali, nchi itakuwa imepoteza fursa ya kupata fedha za ujenzi wa bwawa hili.

**Msheshimiwa Spika,** ili kufanikisha upatikanaji fedha za ujenzi wa Bwawa hili, Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha na masharti ya mikopo kutoka katika mabenki yaliyoonyesha nia ya kusaidia ili kukamilisha mapema iwezekanavyo taratibu za makubaliano na Benki hizo ili ujenzi wa mradi huu uweze kuanza katika Mwaka wa Fedha (2017/2018).

**5) Uratibu wa fedha zingine za miradi ya maendeleo shilingi 78,420,000,000**

**Mheshimiwa Spika,** fedha zingine za nje kiasi cha shilingi **78,420,000,000** ambazo hazijajumuishwa kwenye bajeti ya Wizara ya Maji na umwagiliaji zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara za Afya, Elimu na TAMISEMI. Kufuatia umuhimu wa miradi ya maji nchini, Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo na kuwasilisha taarifa kwenye Kamati mapema mwezi Machi

na kabla Kamati aijafanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**6) Umuhimu wa Mfuko wa Taifa Maji katika kuboresha huduma za maji**

Kamati ilipowasilisha maoni yake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilipendekeza Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 kwa kuweka tozo ya shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya petroli. Mapendekezo hayo yangetekelezwa yangewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji ambao ungesaidia kuboresha huduma za maji. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ushauri huu.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**6.1** **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Eng.Gerson H. Lwenge, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Eng. Isack A. Kamwelwe (Mb) pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji**.**

**6.2** **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma,Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb | “ |
| 5. | Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb | “ |
| 6. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | “ |
| 7. | Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb | “ |

8. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb "
9. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
10. Mhe. John John Mnyika, Mb "
11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb "
12. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb "
13. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb "
14. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb "
15. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
16. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
17. Mhe. Abdallah Hamis Ulega, Mb "
18. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
19. Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko, Mb "
20. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb "
21. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb "
22. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
23. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
24. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb "

**6.3** **Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Virgil Mtui,
Ndg. Martha Chassama na Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**6.4** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumiziya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**6.5** **Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Dkt.Christine G. Ishengoma, (Mb)
**MAKAMU MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
**10 MEI, 2017**